

COVID-19 CHANJO

# Wasaidie Watoto kuwa Watoto

Hakikisha mtoto wako amepata chanjo ya Ugonjwa wa COVID-19 ili kuzuia ugonjwa sugu na kuiepusha familia yako kutokana na virusi hivyo.

## Virusi vya Korona kwa Watoto

Ingawa watoto hawajaathiriwa sana na Ugonjwa wa COVID-19 ikilinganishwa na watu wazima, watoto hupata virusi hivyo mara nyingi kama watu wazima na wanaweza kuusambaza kwa wengine. Watoto walio na magonjwa mengine wako katika hatari kubwa ya ugonjwa sugu, lakini karibu theluthi moja ya watoto waliolazwa hospitalini kutokana na ugonjwa huu, hawakuwa na magonjwa mengine hapo awali.

Visa vya Ugonjwa wa COVID-19 miongoni mwa watoto vimeongezeka nchini Marekani, hasa kutokana na kuenea zaidi kwa maambukizi ya virusi vya aina ya Delta.

Ingawa ni nadra sana, baadhi ya watoto ambao wamekuwa na Ugonjwa wa COVID-19 wanaweza baadaye kupata Ugonjwa wa Uvimbe Sehemu Mbalimbali za Mwili wa Watoto (MIS-C), hali ambayo ni adimu lakini inahatarisha maisha inayohusishwa na Ugonjwa wa COVID-19. Hali hii inaweza kusababisha sehemu mbalimbali za mwili kuvimba, ikiwa ni pamoja na moyo, mapafu, figo, ubongo, ngozi, macho, au viungo vya utumbo.

"Kukiwa na takriban watoto 480,000 wenye umri wa miaka 5-11 kote Colorado, chanjo iliyoenezwa kote ndio njia bora ya kuwalinda watoto kutokana na Ugonjwa wa COVID-19 na kusaidia kumaliza janga hili. Watoto ambao wamechanjwa wanaweza kuhudhuria shule au huduma za watoto kwa usalama zaidi, kukusanyika na familia na marafiki na kufurahia shughuli nyingine mbali na nyumbani. Watoto wanapaswa kuwa watoto, na kuidhinishwa kwa chanjo ya ugonjwa huu kwa kikundi hiki cha umri ni hatua ya kusisimua kwa familia na jamii.

## Hakikisha Mtoto Wako Amepata Chanjo ili Kuzuia Ugonjwa wa COVID-19

- Kituo cha Kuthibiti Magonjwa (CDC) kinapendekeza kwamba kila mtu aliye na umri wa miaka 5 na zaidi apate chanjo ya Ugonjwa wa COVID-19 ili kusaidia kujikinga dhidi ya ugonjwa huo. Watoto walio na umri wa miaka kati ya 5-11 sasa wanaweza kupata chanjo ya Pfizer- BioNTech ya Ugonjwa wa COVID-19.
- Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya Ugonjwa wa COVID-19 kwa watoto ni mfululizo wa dozi mbili zinazotolewa zikiachana kwa wiki tatu (siku 21)i. Kiwango cha chanjo kwa watoto (mikrogramu 10) ni theluthi moja ya kipimo cha chanjo kinachotumiwa kati ya watu wenye umri wa miaka 12+ (mikrogramu 30). Ni muhimu kumpa mtoto wako chanjo kwa kipimo sahihi kulingana na umri wake wakati wa chanjo.
- Chanjo kwa watoto wenye umri wa miaka 5-11 ilikuwa na ufanisi wa asilimia 91% katika kuzuia dalili za maambukizi ya Ugonjwa wa COVID-19, na asilimia 100% ya ufanisi katika kuzuia magonjwa na vifo vikali. Mfumo wa kinga wa watoto wenye umri wa miaka 5-11 ulikuwa na nguvu kama ule ya watu wenye umri wa miaka 16-25.
- Usalama wa chanjo hiyo ulifanyiwa utafiti katika takriban watoto 3,000 wenye umri wa miaka 5-11 ambao walipata chanjo hiyo na hakuna madhara makubwa ambayo yamegunduliwa katika utafiti unaoendelea.
- Madhara baada ya kupata chanjo (dalili za kawaida kwamba mwili wako unajenga ulinzi) miongoni mwa watoto ni sawa na yale ya watu wazima. Madhara ya kawaida ni pamoja na maumivu kwenye sehemu ya kudungwa sindano, uchovu, na maumivu ya kichwa. Madhara haya yanaweza kuathiri uwezo wa mtoto wako kufanya shughuli za kila siku, lakini yanapaswa kutoweka baada ya siku chache. Hakukuwa na madhara makubwa yaliyoonekana wakati wa utafiti wa kimatibabu kwa watoto wa miaka 5-11.
- Chanjo za Ugonjwa wa COVID-19 na chanjo zingine, kama vile mafua au chanjo zingine za kawaida za utotoni, zinaweza kutolewa kwa pamoja.

Tri-County Health Department

Jifunze mengi kuhusu chanjo hii kupitia kwa www.tchd.org/COVIDvaccine

# Vidokezo vya Kumtayarisha Mtoto Wako Kwa Chanjo Yao ya Ugonjwa wa COVID-19

Kama mzazi au mlezi, unaweza kumtayarisha mtoto wako kwa ajili ya chanjo yake ya Ugonjwa wa COVID-19.



### Kabla ya Chanjo:

- Watoto walio na umri wa chini ya miaka 18 wanahitaji idhini ya mzazi ili kupata chanjo. Zungumza na mtoa huduma wako ili kuona kama unapaswa kuwepo kwenye miadi ya chanjo ya mtoto wako au ikiwa unatoa idhini ya mzazi kupitia simu au kwa maandishi.
- Zungumza na mtoto wako kabla ya kupata chanjo kuhusu anachotarajia.

### Wakati wa Chanjo:

- Wahudumu wa afya, wazazi na watoto wenye umri wa miaka 2+ wanapaswa kuvaa barakoa inayofunika pua na mdomo wao.
- Unapaswa kupokea karatasi iliyo na maelezo zaidi na ya kweli kuhusu chanjo ya Pfizer-BioNTech. Kagua taarifa na umuulize mhudumu wa afya kuhusu maswali au wasiwasi wowote unaoweza kuwa nao.
- Mweleze daktari au muuguzi kuhusu mzio wowote ambao mtoto wako anao.
- Unapaswa kupewa kadi ya chanjo ambayo ina maelezo kuhusu mtoto wako alipokea chanjo gani ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona, tarehe aliyoipokea na mahali alipoipokea. Hifadhi kadi hii ya chanjo kwa dozi ya pili ya mtoto wako na ikiwa unaweza kuihitaji kwa matumizi ya baadaye.
- Baada ya chanjo ya mtoto wako ya Ugonjwa wa COVID-19, utaombwa kusubiri kwa dakika 15-30 ili mtoto wako aweze kuangaliwa iwapo atakuwa na athari ya mzio inayohitaji matibabu.
- Uliza mtoa huduma wa afya wa mtoto wako kuhusu kuanza kutumia v-safe, zana ya simu isiyolipishwa inayotumia ujumbe mfupi wa maandishi na uchunguzi wa wavuti ili kutoa ukaguzi wa kibinafsi wa afya baada ya mtoto wako kupokea chanjo ya Ugonjwa wa COVID-19. Kupitia v-safe, unaweza kuripoti madhara yoyote ambayo mtoto wako anaweza kuwa nayo baada ya chanjo. V-safe pia inakukumbusha wakati mtoto wako atapokea dozi ya pili. Jifunze mengi kuhusu v-safe.

### Baada ya chanjo:

- Fuatilia madhara yoyote baada ya chanjo, hasa wakati wa wiki ya kwanza baada ya chanjo. Madhara mengi ni ya kawaida na yanapaswa kutoweka ndani ya siku chache. Watu wengine hawapati madhara yoyote. Wasiliana na daktari wako au mtoa huduma ya afya ikiwa: :
  - » Wekundu au uchungu mahali ulipodungwa utazidi kuwa mbaya baada ya saa 24
  - » Madhara yako yanakupa wasiwasi au hayaonekani kutoweka baada ya siku chache
  - » Ikihitajika, zungumza na mtoa huduma wa afya wa mtoto wako kuhusu kuchukua dawa za dukani, kama vile ibuprofen, acetaminophen au dawa zingine zisizo za aspirini, kwa maumivu na usumbufu wowote baada ya kupata chanjo.
  - » Kumbuka kumpeleka mtoto wako kupokea chanjo ya pili, wiki tatu (siku 21) baada ya dozi yake ya kwanza.

## Jinsi ya Kumpa Mtoto Wako Chanjo ya Ugonjwa wa COVID-19

Wasiliana na mtoa huduma wa afya ya mtoto wako, duka la dawa la karibu au kliniki.

**Tembelea tovuti ya Jimbo kwa watoa huduma**
covid19.colorado.gov/kids-vaccines

**Pata orodha kamili ya watoa huduma kwenye**
bit.ly/CDPHEvaccineProvider

Tri-County Health Department

Jifunze mengi kuhusu chanjo hii kupitia kwa www.tchd.org/COVIDvaccine